



AZIMIO NA. 09/2017

AZIMIO LA BUNGE LA KURIDHIA ITIFAKI YA NYONGEZA YA TANO YA MWAKA 1994, ITIFAKI NYONGEZA YA SITA YA MWAKA 1999, ITIFAKI YA NYONGEZA YA SABA YA MWAKA 2004, ITIFAKI YA NYONGEZA YA NANE YA MWAKA 2008 NA ITIFAKI YA NYONGEZA YA TISA YA MWAKA 2016 YA KATIBA YA UMOJA WA POSTA DUNIANI (*FIFTH ADDITIONAL PROTOCOL OF 1994, SIXTH ADDITIONAL PROTOCOL OF 1999, SEVENTH ADDITIONAL PROTOCOL OF 2004, EIGHTH ADDITIONAL PROTOCOL OF 2008 AND NINTH ADDITIONAL PROTOCOL OF 2016 TO THE CONSTITUTION OF THE UNIVERSAL POSTAL UNION*).

KWA KUWA, Umoja wa Posta Duniani (*Universal Postal Union-UPU*) ni Wakala wa Umoja wa Mataifa (UN) ulioundwa kwa mujibu wa Katiba ya Umoja huo kwa madhumuni makuu ya kukuza mawasiliano miongoni mwa nchi wanachama kwa kutoa huduma bora za posta ili kufikia malengo ya kimataifa katika nyanja za kiutamaduni, kijamii na kiuchumi;

NA KWA KUWA, Sekta ya Posta imekuwa ikikabiliwa na changamoto mbalimbali zitokanazo na maendeleo ya kiteknolojia, utandawazi na soko huria hali iliyosababisha Katiba ya UPU kufanyiwa marekebisho kila baada ya miaka minne wakati wa Mikutano Mikuu ya UPU;

NA KWA KUWA, kwa mujibu wa Ibara ya 30 ya Katiba hiyo tajwa, marekebisho hayo huunda Itifaki Nyongeza (*Additional Protocols*) ya Katiba kwa lengo la kuirekebisha ili kuziwezesha nchi wanachama kukabiliana na changamoto zilizopo na kuifanya Sekta ya Posta kuongeza mchango wake katika maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii;

NA KWA KUWA, marekebisho ya Katiba ya Umoja wa Posta Duniani yaliyotokana na Itifaki Nyongeza ya Tano ya Seoul, Korea ya Kusini ya mwaka 1994; Itifaki Nyongeza ya Sita ya Beijing, China ya mwaka 1999; Itifaki Nyongeza ya Saba ya Bucharest, Romania ya mwaka 2004; Itifaki Nyongeza ya Nane, Geneva, Uswisi ya mwaka 2008 na Itifaki Nyongeza ya Tisa ya Istanbul, Uturuki ya mwaka 2016 yalikubaliwa katika Mikutano Mikuu ya miaka iliyotajwa;

NA KWA KUWA, Tanzania ilishasaini Itifaki nyongeza hizi na hatua inayofuata ni kuridhia ili kuendelea kunufaika na haki za Umoja kama Nchi Mwanachama;

NA KWA KUWA, licha ya kutoridhika Itifaki hizo, Tanzania imeendelea kutimiza kikamilifu masharti mengine ya Katiba na Masharti ya uanachama ikiwa ni pamoja na kulipia ada ya uanachama na kushiriki katika mikutano mbalimbali ya umoja huo na kuchaguliwa katika nyadhifa mbalimbali;

NA KWA KUWA, kwa mujibu wa Ibara za 25 na 26 za Katiba ya UPU, nchi wanachama zilizosaini marekebisho ya Katiba yaliyotokana na Itifaki Nyongeza zinatakiwa kuridhia kulingana na utaratibu wa nchi husika;

NA KWA KUWA, kwa kuridhiwa kwa Itifaki hizi na nchi wanachama zitaweka mwongozo wa namna ya mabadiliko ya kutenganisha Posta kutoka Simu (*Postal reform-separation of Post Telecommunication*) hivyo kuboresha shughuli za Posta na kuinua ufanisi wake;

NA KWA KUWA, kuridhiwa kwa Itifaki hizo na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutaiwezesha Posta kutoa huduma kwa umma kwa ubora na kwa wakati na kuingia katika mfumo muafaka wa ushindani;

NA KWA KUWA, kuridhiwa kwa Itifaki hizo na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutaweka mfumo mpana zaidi unaojumuisha mifumo ya kielektroniki kwa ajili ya utumaji wa fedha kupitia mashirika ya Posta ambao Tanzania imeingia makubaliano;

NA KWA KUWA, kuridhiwa kwa Itifaki kutafanya uwepo utaratibu mpya wa kukokotoa malipo ya mrahaba kutokana na kusambaza barua kutoka

nchi nyingine (*terminal dues*) unaowezesha kuwepo kwa mfuko maalum wa fedha za miradi na vitendea kazi;

HIVYO BASI, kwa kuzingatia manufaa yatokanayo na Itifaki hii, Bunge hili katika Mkutano wa Nane na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka, 1977 linaazimia kuridhia Itifaki ya Nyongeza ya Tano ya Mwaka 1994, Itifaki Nyongeza ya Sita ya Mwaka 1999, Itifaki Nyongeza ya Saba ya Mwaka 2004, Itifaki ya Nyongeza ya Nane ya Mwaka 2008 na Itifaki ya Nyongeza ya Tisa ya Mwaka 2016 ya Katiba ya Umoja wa Posta Duniani ili Tanzania iweze kushirikiana na nchi nyingine za Umoja huu katika kukuza maendeleo ya huduma za Posta Afrika (***Fifth Additional Protocol of 1994, Sixth Additional Protocol of 1999, Seventh Additional Protocol of 2004, Eighth Additional Protocol of 2008 and Ninth Additional Protocol of 2016 to the Constitution of the Universal Postal Union***).

Limepitishwa na Bunge leo tarehe 8 Septemba, 2017.

Dkt. Thomas D. Kasilillah
KATIBU WA BUNGE